**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

SHULE YA SEKONDARI SUBIRA
S.L.P 882
SONGEA

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO KIDATO CHA KWANZA – 2021

MZAZI/MLEZI WA:

........................................................................................................................................

Ninayofuraha kubwa kukujulisha kuwa:

1. Mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari ya Subira. Shule hii ni ya kutwa na mchanganyiko wa wavulana na wasichana. Shule ya Sekondari Subira ipo katika Manispaa ya Songea, katika kata ya Subira upande wa Magharibi mwa Mji barabara iendayo Mpitimbi.
2. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021. Unatakiwa umlete mwanao shuleni siku hiyo saa moja na nusu (1:30) asubuhi bila kukosa.
3. Yafuatayo ni maagizo muhimu ya kujiunga na shule hii. Hivyo yasome kwa makini uyaelewe na uyatekeleze ili mwanao apokelewe shuleni.

3.1: SARE ZA SHULE

A. WAVULANA
   i. Viatu vyeusi vya ngozi pea mbili, vyenye kisigino kifupi na viwe ni vya kamba
   ii. Soksi nyeusi pea mbili
   iii. Shati mbili nyeupe za mikono mifupi
   iv. Suruali mbili za rangi ya damu ya mzee, kitambaa kimeambatanishwa.
   v. Tai ya rangi ya damu ya mzee yenye utepe mweupe mmoja kwa kidato cha kwanza
   vi. Sweta la rangi ya damu ya mzee iliyokatwa V shingoni.
   vii. Vifaa vya michezo (raba nyeusi na Tracksuit nyeusi)

B. WASICHANA
   i. Viatu vyeusi vya ngozi pea mbili, vyenye kisigino kifupi na viwe ni vya kamba
   ii. Soksi nyeupe pea mbili
   iii. Shati mbili nyeupe za mikono mifupi
   iv. Sketi mbili ndefu kutosha za rangi ya damu ya mzee, malinda ya kupanga(sio linda box) kitambaa kimeambatanishwa, **(sketi fupi haziruhusiwi kuvaliwa shuleni)**
   v. Tai ya rangi ya damu yam zee yenye utepe mweupe mmoja kwa kidato cha kwanza
   vi. Sweta rangi ya damu ya mzee yenye V shingoni.
   vii. Vifaa vya michezo (raba nyeupe na Tracksuit nyeusi)

Scanned with CamScanner

4. MAHITAJI MENGINE

i. Begi/Mkoba wa kubebea madaftari (SIO KIFUNGASHIO)
ii. Madaftari (COUNTER BOOKS 10 QUIRE 3)
iii. Mkebe mmoja (Mathematical set)
iv. Kamusi ya Kiingereza (Dictionary)
v. Viandikio kama peni, penseli, rula , mfuto vya kutosha.

NB: Ni vizuri Mzazi umuandae vyema mtoto wako pamoja na mahitaji yote muhimu ili asihangaike awapo darasani. Hakikisha mtoto wako anaripoti shuleni kwa muda uliopangwa. HAKUNA SABABU ITAKAYOSIKILIZWA DHIDI YA MWANAFUNZI ASIYERIPOTI SHULENI, HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA KWA MZAZI AU MLEZI HUSIKA.

*Marufuku mwanafunzi KUMILIKI AU KUTUMIA SIMU awapo shuleni*

5. VIAMBATANISHO

a) Fomu Na. "B" ipelekwe Hospitali ya Serikali ya MJIMWEMA pekee na sio mkoani wala Subira Zahanati kwa ajili ya mwanao kupimwa afya yake, ni lazima.
b) Fomu Na. "C" ijazwe kwa ajili ya kutujulisha kukubali au kutokubali kupokea nafasi ya kujiunga na kidato cha kanza katika shule hii na zirudishwe shuleni.
c) Sheria na kanuni za shule

Nakutakia maandalizi mema na KARIBU SANA

MKUU WA SHULE
SUBIRA SEKONDARI
S. L. P. 882
SONGEA

.................................

SANGA, G
MKUU WA SHULE
0754 442 323/ 0716 767 327

MOTTO WETU: " DAIMA MBELE, NYUMA MWIKO"

Scanned with CamScanner

FOMU "B"

*(ijazwe na irudishwe shuleni siku ya kuripoti mwanafunzi)*

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

From SUBIRA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 882
**SONGEA**

Date …………20 ……….

**Part A:**

To the Medical Officer,

……………………………………………………………………………………………………………

Student's Name ………………………………………………………………………… *(Name in full)*

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time Student. The examination should include the following Categories (I – III), each category or sub – category of which will render the applicant ineligible in case of a defect.

**Part B: Medical certificate**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time student of Secondary education

1. a) Eye – sight ……………………………………………………………………
   b) Hearing ……………………………………………………………………
   c) Limbs ……………………………………………………………………
   d) Speech ……………………………………………………………………
   e) Venereal diseases ……………………………………………………………
   f) Leprosy ……………………………………………………………………
   g) Epilepsy ……………………………………………………………………
   h) Pregnancy ……………………………………………………………………
   i) Stool ……………………………………………………………………
   j) Urine ……………………………………………………………………
   k) Blood Pressure ……………………………………………………………
2. Neuroses ……………………………………………………………………
3. Other serious diseases ……………………………………………………

Date: ……………………………… Signature: ……………………………………

Station: ……………………… .. Designation: ……………………………………

MKUU WA SHULE
SUBIRA SEKONDARI
S. L. P. 882
SONGEA

Scanned with CamScanner

FOMU "C"

*(Ijazwe na irudishwe shuleni siku ya kuripoti mwanafunzi)*

**AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU**

Mimi (*Mwanafunzi*) ……………………………………………………………………………………Ninakubali nafasi niliyoipata katika shule ya sekondari ya Subira kuendelea na masomo. Nafahamu kuwa ninagharamiwa na Taifa linalothamini kazi na juhudi. Naahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa upeo wa uwezo wangu kuwa Mwanafunzi mwema. Ninaahidi kutoshiriki katika mambo yatakayosababisha Mwanafunzi kuachishwa shule. Naahidi kuwa nitashirikiana na walimu pamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa shule na Taifa kwa ujumla.

……………………………………………

Sahihi ya Mwanafunzi

Mimi(*Mzazi/Mlezi*) ………………………………………………………………………………………Nimesoma maelekezo yote na kuyaelewa.Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyoagizwa katika barua hii. Ripoti na barua zote zinazomhusu mtoto wangu ziletwe kwangu kwa anwani (*Andika Anwani Yako hapa*)

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………

Jina la Mzazi/mlezi…………………………………………………… Sahihi ya mzazi/mlezi………………………

Namba ya simu ya mzazi/mlezi………………………………………Tarehe……………………………………

**NDUGU WA KARIBU:**

Hakikisha unaandika majina matatu na namba zao za simu. Hii inasaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo linatokea, hatutaki majina ya ndugu wa bandia.

1. a)Jina ……………………………………………………………………………………………
   b) Uhusiano ………………………………………………………………………………………
   c) Namba ya simu …………………………………………………………………………………
2. a) Jina ……………………………………………………………………………………………
   b) Uhusiano ………………………………………………………………………………………
   c) Namba ya simu …………………………………………………………………………………
3. a) Jina ……………………………………………………………………………………………
   b) Uhusiano ………………………………………………………………………………………
   c) Namba ya simu …………………………………………………………………………………

Hango!

MKUU WA SHULE
SUBIRA SEKONDARI
S.L.P. 8[illegible]2
SONGEA

Scanned with CamScanner

# SHULE YA SEKJONDARI YA SUBIRA
# SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

## A. HESHIMA

1. Mwanafunzi asimame na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita,darasani au kwenye ukumbi wa mkutano.
2. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yake na wenzake, kwa walimu wake na kwa watu wengine
3. Wanafunzi awaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake
4. Mwanafunzi ashirikiane na kusaidiana na wenzake kaika kazi
5. Mwanafunzi athamini na kuheshimu kazi za aina zote
6. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo
   a. Kuvuta sigara
   b. Kufuga kucha ndefu
   c. Kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi
   d. Kufuga ndevu
   e. Kuvaa mavazi yasiyo na heshima
   f. Kugombana
   g. Kuvaa mlegezeo

7. Mwanafunzi aitike mara moja kukimbilia aliko mkuu anayemwita
8. Mwanafunzi aheshimu bendera ya Taifa (Serikali) picha za viongozi na Wakuu wa Serikali.Nembo ya Taifa (Coat of Arms). Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa
9. Mwanafunzi aheshimu na kutunza ukumbi wa mikutano mahali pa kulia chakula ofisi za shule mali binafsi na mali ya umma
10. Mwanafunzi anatakiwa kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma
11. Mwanafunzi awe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote alipo
12. Mwanafunzi anyooshe mkono juu na kusimama anapoulizwa na kujibu maswali
13. Mwanafunzi akae kimya wakati wote anapokuwa darasani, asitoke bila ya hurusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko

Scanned with CamScanner

## B. MAHUDHURIO

1. Mwanafunzi ahudhurie shule kwa muda wote wa masomo
2. Mwanafunzi ahudhurie vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa
3. Mwanafunzi ahudhurie katika kazi zote za mikono
4. Mwanafunzi ahudhurie mikutano ya shule kama Baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa na mikutano mingine
5. Kila Mwanafunzi atapaswa kufuata Dini amabayo wazazi wake wanaikubali, kubadili dini ukiwa shuleni bila ridhaa ya wazazi haitaruhusiwa
6. Mwanafunzi anaposhindwa kuhudhuria masomo au shughuli nyingine ya kishule kwa sababu ya UGONJWA lazima atoe taarifa kwa mwalimu wa zamu au mwalimu wa darasa ili ampatie kibali cha kwenda kutibiwa na lazima aonyeshe cheti cha mganga kwa mwalimu wa zamu au wa darasa baada ya kutibiwa.
7. Mwanafunzi aliyeomba ruhusa akifika nyumbani aonyeshe kibali cha ruhusa alichopewa shuleni na mzazi atie saini yake na kibali hicho kirudishwe shuleni. **MTOTO WAKO ASIPOKUONYESHA KIBALI CHA RUHUSA UJUE KATOROKA.**

## C. KUWAHI

1. Mwanafunzi awahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya shule
2. Mwanafunzi atii mlio wa kengele na kuwahi anapohitajika

## D. SARE YA SHULE

1. Kila Mwanafunzi atavaa sare ya shule:
   a) Wakati wote wa masomo ya darasani
   b) Wakati wote wa mihadhara ya shule (Baraza)
   c) Wakati wa kwenda hospitalini au kwenye maandamano
   d) Wakati wa kwenda nyumbani
2. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa vitu vifuatavyo pamoja na sare ya shule
   a) Viatu vya ghorofa
   b) Kofia (kepu) isipokuwa kwa waislamu wakati wa kwenda msikitini kuswali
   c) Mapambo mengine yoyote kama hereni, pete, mkufu, culture, bangili, vibanio vya nywele, n.k.

## E. MIPAKA YA SHULE

1. Mwanafunzi haruhusiwi wakati wa kuwa shuleni kuwa nje ya mipaka ya shule bila kibali maalum.
2. Mwanafunzi atatembelea sehemu zifuatazo kwa kibali maalum:
   a) Ofisi za shule
   b) Maabara
   c) Jikoni
   d) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
3. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:
   a) Vilabu vya pombe
   b) Majumba ya starehe kama vile kumbi za disko
   c) Majumba ya kufikia na kulala wageni

## F. USAFI

Usafi ni wajibu wa kila Mwanafunzi katika sehemu ya maisha yake ya kila siku. Kwa hiyo kila Mwanafunzi atazingatia yafuatayo

a. Usafi wa mwili wake na nguo zake
b. Usafi wa ukumbi wa chakula
c. Vyakula viliwe ndani ya bwalo la chakula tu.
d. Usafi wa vyoo, madarasa, maabara, viwanja na barabara

Scanned with CamScanner

## G. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi wa vitu na wizi wa kalamu (forgery)
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji wa bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupiga au kupigana
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ta Taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani ya shule na nje ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani
13. Kukataa adhabu kwa makusudi

**ELIMU NA NIDHAMU HUENDA PAMOJA**

..............................

**SANGA, G.**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SUBIRA SEKONDARI
S. L. P. 882
SONGEA

Scanned with CamScanner